*Kioo cha Lugha*
*Juzuu 1, Na. 2 (1995)*

# MAPITIO YA KITABU*

JINA: **Walenisi** (kurasa 190)
MTUNZI: Katama Mkangi
Mchapishaji: East African Educational Publishers, Nairobi(1995)
Mpitiaji: Mwenda Mbatiah.

## 1.0 Utangulizi

Jina la Katama Mkangi lilianza kuvuma katika ulimwengu wa fasihi ya Kiswahili hasa nchini Kenya mwaka wa 1975. Huo ndio mwaka ambapo kazi yake ya kwanza, **Ukiwa**, ilipochapishwa. Kazi hiyo ni hadithi ya mapenzi kati ya vijana wawili: Lila na Matano. Mapenzi yao yanadumu kwa muda wa miaka kadhaa mpaka Lila anapoondoka kwenda masomoni Nairobi ambapo anamsahau Matano. Hadithi inaishia kwenye tanzia kwa kuwa baada ya kukaa Nairobi kwa miezi michache Lila anakufa kutokana na ajali ya barabarani. Kazi ya pili ya Mkangi ni **Mafuta** iliyochapishwa mwaka wa 1984. Kazi hiyo inayobainisha maonevu ya kisiasa na kiuchumi dhidi ya wananchi walio wengi ndiyo inayomtambulisha Mkangi kama mwandishi ambaye amedhamiria kukuza fasihi ya kiukombozi. Mapendeleo yake ya kisiasa, hasa suala la ukombozi, yanafikia kilele chake katika riwaya pevu ya **Walenisi.**

Mwandishi alizaliwa 20 Machi, 1944 kule Ribe katika Mkoa wa Pwani nchini Kenya. Yeye ni mtaalamu aliyepata digrii ya juu ya Ph.D katika taaluma ya sosholojia katika Chuo Kikuu cha Sussex. Baadaye alikuwa mhadhiri katika Idara ya Sosholojia, Chuo Kikuu cha Nairobi. Mihadhara yake ilipendwa sana na wanafunzi pamoja na wahadhiri wenzake kwa sababu, mbali na uhodari wake kama mwanasosholojia, alipenda kuzungumzia masuala nyeti ya kijamii na kisiasa nchini Kenya. Masuala hayo yaliwaathiri Wakenya wengi kwa njia moja au nyingine, lakini wengi wao waliogopa kuyazungumzia kwa sababu ya mazingira ya kisiasa yaliyotawala wakati huo. Mazungumzo na mawazo yake yaliyojitokeza katika makala zake nyingi zilizochapishwa magazetini (na zinazoendelea kuchapishwa hata sasa) vilibainisha chuki yake dhidi ya mfumo wa kibepari nchini Kenya. Mwandishi huyo alitiwa kizuizini mwaka wa 1986. Waliomfunga walidai kuwa alihusika na kundi la siri la Mwakenya lililotaka kuiangusha serikali. Hata hivyo, Wakenya wengi waliamini kuwa kufungwa kwake kulitokana na mawazo, itikadi na msimamo wake ambao ulipingana na ule wa watawala. Baada ya kuachiliwa kutoka kizuizini Mkangi alinyimwa kazi katika vyuo vikuu vya kitaifa. Kwa hivi sasa anafunza katika Chuo Kikuu cha USIU jijini Nairobi.

## 2.0 Muhtasari wa Hadithi

Hadithi ya **Walenisi** ni juu ya Dzombo ambaye ni mtu mdadisi apendaye kujua asili ya mambo. Udadisi wake na kupenda kwake ukweli ndiyo mambo yanayomchongea kwa sababu utawala dhalimu wa nchi yake haupendi watu wadadisi na wanaofichua ukweli. Watu kama hao wanachukuliwa kuwa ni wachochezi na wanaohatarisha utulivu katika jamii. Matatizo ya Dzombo yanaanza anapomfichulia nduguye ukweli kwamba ufukara wao umetokana na kunyonywa na tajiri wanayemfanyia kazi. Habari hizo zinapomfikia tajiri wao, Dzombo anafutwa kazi kwa "kuwachochea wafanyikazi watiifu." Baadaye Dzombo anaamua kujiajiri mwenyewe katika kilimo. Analima kwa bidii na kupanda mahindi ili ajipatie chakula na mahitaji mengine. Mahindi yake yanamea vizuri. Lakini kwa kuyapanda, anakwenda kinyume na sera ya nchi yake. Viongozi wa nchi hiyo wameagizwa na mataifa makuu ya kibepari kupitia Benki ya Dunia kuhakikisha kwamba nchi hiyo inatoa tu mazao ya biashara k.v. katani, pareto, kahawa na kakao, ambayo yatauzwa kwa mataifa hayo. Kwa hivyo mahindi ya Dzombo yanafyekwa na analazimika kupanda

mazao yaliyopendekezwa. Anafuata maagizo hayo, lakini anapovuna na kupeleka mavuno yake kwenye Idara ya Serikali inayohusika, halipwi chochote. Anaambiwa kuwa bei ya mazao hayo katika masoko ya nje imeteremka. Dzombo anapozidi kukosoa na kudadisi, anakamatwa na kupelekwa mahakamani ambako anahukumiwa kifo.

Katika nchi hiyo, kuna njia ya kipekee ya kuwaangamizia watu waliohukumiwa kifo. Wanatiwa kwenye chombo kiitwacho "Sayari" ambacho kinarushwa kama roketi kwenda anga za juu na kisha kulipuka na hivyo kumuua anayehusika. Lakini Dzombo ananusurika kwa kuwa chombo kinaporushwa angani anaushika usukani wake na kukiendesha mwenyewe. Badala ya kulipuka, chombo kinapaa angani na hatimaye kutua katika Sayari nyingine. Dzombo anagundua kwamba hii ni sayari ya kiparadiso iliyojaa mema na inayoendeshwa katika misingi ya usoshalisti. Wenyeji wake wanamtembeza katika nchi yao ijulikanayo kama **Walenisi**. Dzombo anashangaa sana kuona jinsi nchi hiyo ilivyopiga hatua kabisa katika sekta zote. Anaona kuwa kila kitu ni kinyume cha nchi yake ambayo imejaa umaskini na dhuluma. Baadaye Dzombo anamuoa mwanamke wa Kiwalenisi. Hadithi inaishia kwenye makubaliano baina ya Dzombo na mkewe, akiwa na mimba ya miezi mitatu, kwamba watafunga safari kwenda alikotoka Dzombo ili kuikomboa nchi hiyo na kuanzisha mfumo wa Kiwalenisi.

### 3.0 Maudhui na Fani

**Walenisi** ni tahakiki ya mfumo wa kibepari pamoja na tafakuri juu ya mfumo ufaao katika kuwalea wanadamu waliokamilika kiutu. Kwa hiyo suala kuu linaloshughulikiwa katika kazi hii ni utu. Maovu ya kibepari yanajitokeza katika mashaka makubwa yanayomfika Dzombo, ambaye ni mwananchi wa kawaida anayejaribu kuishi kwa kutegemea jasho lake. Juhudi zake za kuyajenga maisha yake kwa njia halali zinaangamizwa na watawala wanaodumisha mfumo ambao unawanufaisha wao na kuwanyima watu wa kawaida walio wengi haki zao za kibinadamu.

Jamii ya Dzombo imejengeka katika misingi ya ubepari uchwara unaotawala nchi nyingi za Kiafrika. Ubepari huo ni matokeo ya ukoloni mamboleo. Enzi ya ukoloni huo ilianza pale ambapo mataifa yaliyoigawa Afrika na kuitawala kikoloni yalitoa uhuru wa bandia na kuwakabidhi uongozi vikaragosi wao wa Kiafrika. Mataifa hayo yanaendelea kuitawala Afrika kiuchumi kupitia vikaragosi hao. Katika hali hii, sera za makoloni mamboleo kisiasa na kiuchumi ni ufuataji wa maagizo yanayotolewa na mataifa makubwa ya kibepari kupitia vyombo vyao, kwa mfano Benki ya Dunia. Maagizo hayo hayadhamiriwi kuwafidia wananchi wa nchi maskini bali kuendelea kupanua uchumi wa mataifa hayo makubwa.

Mazao ambayo wananchi kama Dzombo wanalazimika kupanda ni yale yenye kutoa malighafi ya viwanda vya mataifa makuu ya kibepari. Serikali ya nchi anamoishi Dzombo haijali hata wananchi wakifa njaa kutokana na kutopanda mimea ya chakula, bora itimize maagizo ya mabwana wao kutoka nje. Kutokana na hayo tunaona kwamba:

(a) Nchi za Kiafrika ni maskini kwa sababu uchumi wao hudhibitiwa na mataifa ya kibepari yaliyoendelea.

(b) Mfumo wa ubepari uchwara unaofuatwa na nchi maskini za Kiafrika unalinufaisha kundi dogo tu la watawala huku wananchi walio wengi wakizidi kuzama katika umaskini na dhuluma za kila aina.

Matokeo ya yote hayo ni jamii ambazo zinauangamiza utu badala ya kuujenga na kuudumisha. Kuhukumiwa kifo kwa Dzombo katika mazingira ambayo tumeyaeleza hapo juu ni ishara ya utovu wa utu katika jamii yake. Tajiriba ya Dzombo anapokuwa katika nchi ya Walenisi inaonyesha kuwa hali ya jamii yake iliyoelezwa hapo juu si lazima iwe ya kudumu. Ni hali inayoweza kubadilishwa ikiwa wananchi walio wengi watachukua hatua za kuibadilisha. Mabadiliko yanayotokea Walenisi baada ya nchi hiyo kutoka kwenye mfumo wa ubepari hadi mfumo wa usoshalisti yanaonyesha kuwa maisha ya wanadamu popote walipo yanaweza

kuboreshwa kwa kuung'oa ubepari na kuujenga usoshalisti. Mfumo wa kisoshalisti ndio unaoweza kuleta usawa na kuhakikisha kwamba watu wote wanatendewa haki.
Riwaya nzima imejikita kwenye "ndoto" - safari ya kindoto ya Dzombo kwenda Walenisi - nchi ya kindoto, na tajiriba za kindoto za Dzombo huko Walenisi.

Jina la nchi hiyo ya kindoto iitwayo Walenisi ni la kiistiara na linasisitiza kanuni ya kisoshalisti ya umoja katika kuyatatua matatizo ya kijamii na moyo wa kusaidiana. Tunaelezwa kuwa maana ya Walenisi ni kwamba "wale ni sisi na sisi tu wale..." (uk. 171). Akimfafanulia Dzombo maana ya jina la nchi yao, Matu Nasi anamweleza kuwa jina hilo linasisitiza usemi kwamba "maslahi yangu na ya wenzangu hayabandukani" (uk. 128). Hata majina ya watu yanatilia mkazo itikadi ya udugu, usawa na utu. Dzombo anapowasili Walenisi anapewa jina la Mtu-Dzombo. Wenyeji wake nao ni Mzee Mtu-Mwenzio na Mama Mtu-Maanani, pamoja na watoto wao: Mtu-Bint Fikirini, Mtu-Wazo, Mtu-Bint Hekima na Mtu-Tabia.

Dhamira ya utu imejengwa kwa kukaririwa kwa dhana ya utu. Kukaririwa kwake kunaifanya dhana hiyo kuwa motifu muhimu zaidi riwayani. Ifuatayo ni baadhi ya miktadha ambapo motifu hiyo inajitokeza:

1. Safari ya Dzombo kuzuru nchi ya Walenisi inaelezwa kama "Safari ya Utu" (uk. 39).
2. Mtu-Bint Fikirini - mchumba wa Dzombo, anamweleza kuwa nchini Walenisi, "sababu ya kwanza ya kuoana ni kutaka kuendeleza utu" (uk. 117).
3. Tunaelezwa kwamba Walenisi ilipopata mwamko wa kimapinduzi uliokuwa chanzo cha mabadiliko makubwa, ndipo utu wa wananchi ulipochipuka (uk. 170).
4. Mzee Mtu-Mwenzio akimweleza Dzombo utaratibu wa utawala wa Walenisi anamwambia kuwa jukumu la viongozi ni kuyakabili matatizo yaliyopo na kuyatatua kwa lengo la kuimarisha utu (uk. 174). Anamweleza pia kuwa "ubaguzi ni utovu wa utu."
5. Uchumi wa Walenisi unaelezwa kama "uchumi wa kiutu" (uk. 178).
6. Mfumo wa kisiasa wa Walenisi unaelezwa kama ambao umejikita katika mapenzi na utu: "Matendo yetu ya kiutu ndiyo mzizi wa mti wetu wa mapenzi", tunaelezwa (uk. 184 - 185).
7. Tunaelezwa pia kuwa "kujua kugawa ndio utu utokao rohoni na kunyeshea mapenzi" (uk. 187).
8. Baada ya Dzombo kuufahamu mfumo wa kisiasa wa Walenisi, tunaelezwa: "... Dzombo akawa amegundua utu wake" (uk. 188).
9. Dzombo akimweleza mkewe athari za tajiriba yake akiwa **Walenisi**, anasema: "lakini ni kweli kiko kinachonisumbua; nacho kimesababishwa na ufahamu wa kiutu" (uk. 189).

Tashibiha inayolinganisha hali hiyo na maumbile ya popo inatumiwa ili kuonyesha utokawaida wake. Dzombo anasema: "N kama popo, tunaonea gizani tu. Ukweli ni kwamba popo ni vipofu; nasi pia ni vipofu!" Anaona kuwa hali hiyo ya "upopo" ni kinyume cha hali ilivyo nchini Walenisi. Anaendelea kusema: "... Tungekuwa binadamu tungeona kama hawa **Wawalenisi...**" (uk. 123).

Ili kusisitiza ubovu wa jamii ya Dzombo, jazanda ya jehanamu inatumiwa. Dzombo anapofika **Walenisi** ndipo anapogundua kuwa atokako kwa hakika sio duniani bali ni jehanamu. Akiwa duniani hangeweza kufahamu hivyo kwa sababu hakuwa na tajiriba ya hali nzuri zaidi (kama ile ya Walenisi). Atokako ni jehanamu kwa kuwa anayetawala huko sio Mungu bali ni Shetani wa pesa/mali/utajiri. Kwa kufafanua jinsi vitu hivyo vitatu vinavyoabudiwa katika jamii yake, Dzombo anaeleza: "Hayo majina matatu ndiyo yanayoeleza utukufu wa Ubaba, Umwana na wa Uroho Mtakatifu" (uk. 71). Katika jamii ya Dzombo, wanawake hawapewi hadhi yoyote bali wanatumiwa kama vyombo vya kutoshelezea ashiki za wanaume. Wafanyikazi nao hawana haki zozote. Ni kama watumwa ambao wanaweza kutendewa chochote na waajiri wao. [ele]ata kazi zenyewe ni adimu na kwa hivyo wale wanaozipata wanashawishika kuamini kwamba wamebahatika na hivyo basi wanapaswa kuwatii wakubwa na waajiri wao ili wasipoteze bahati yao.

Kinyume cha jehanamu ni ahera, na hii ndiyo jazanda inayotumiwa kuuelezea ulimwengu wa Walenisi, ili kuonyesha uzuri wake. Dzombo anapotua Walenisi kwa Sayari, wazo linalomjia akilini ni kwamba amefika mbinguni kwa Mungu. Baada ya kuuonja utamu wa maisha katika ulimwengu huo, anasema kimoyomoyo: "Na ikiwa huku si akhera, basi ni wapi tena?" Tunaelezwa pia kuwa:

Kwa yale machache ambayo alikuwa ameshawahi kuyaona, kutendewa na kusikia, hakukuwa na lolote la upuuzi, la kuonewa, la ubaradhuli, na wala la kujitakia. Ulimwengu huu ulikuwa wa kivyake (uk. 68).

"Safari ya Utu" ya Dzombo inamwezesha kuvumbua utu na hivyo kubadilika kutoka mtu wa duniani (jehanamu) na kuwa Mwalenisi. Ishara ya kubadilika kwake ni kuozwa kwake binti wa Kiwalenisi pamoja na dalili za kuonyesha kuwa watazaa mtoto. Mimba ya Mtu-Bint Fikirini ni ishara ya kizazi kipya kitakachozaliwa baada ya mapinduzi ambayo Dzombo na mkewe wanadhamiria kwenda kuyaanzisha duniani.

## 4.0 Hitimisho

Riwaya huainishika katika makundi mawili makuu, yaani la kiuhalisia na la kiromansi. Riwaya za kiuhalisia ni zile zinazousawiri ulimwengu ambao unalingana na wetu. Riwaya nyingi za Kiswahili ni za aina hii. Romansi ni riwaya ambazo zinatupa picha ya ulimwengu ambao ni tofauti na ulimwengu wetu. Riwaya ya **Walenisi** ni ya aina hii. Mwandishi anasawiri jamii ya kiutopia ambayo ni kinyume cha jamii za ulimwengu halisi wa wanadamu. Lengo lake ni kuonyesha jinsi jamii zetu zilivyo pungufu na mbovu na jinsi utu wetu ulivyofifia. Muhimu zaidi ni kwamba kwa kueleza taratibu zilizofuatwa katika kuijenga jamii hiyo ya kindoto, mwandishi anatwambia kuwa jamii zetu duni zinaweza kubadilishwa, zikaboreshwa kufikia viwango vya juu sana. Mtindo wa kiistiara uliotumiwa unaendana vizuri na maudhui pamoja na malengo ya mwandishi. Kwa kumalizia, ni muhimu kutaja kwamba **Walenisi** ni mojawapo katika riwaya inayoegemea kwenye mtazamo wa ki-Maksi zaidi kuliko riwaya nyingine za Kiswahili. Upendelevu wa kiitikadi unapofikia kiwango kama hiki unateremsha hadhi ya kisanaa ya kazi inayohusika kwa kusheheneza mahubiri katika kazi yake ya sanaa. Hicho ndicho kiini cha udhaifu wa riwaya ya **Walenisi**.

---

*Mapitio mafupi ya riwaya hii yalichapishwa katika *Sunday Nation* (11 Februari, 1996) yakiwa na kichwa: "Brush with the Dark side of Capitalism"